

Kiasi cha Mbegu

Kilo 8 hadi 10 kwa kila eka na mbegu tatu-nne kwa kila shimo. Mimea changa hupaliliwa zibaki moja baada ya wiki mbili.

Undani wa Kupanda

Mbegu zinapandwa sentimita 4 hadi 5 ndani ya mchanga na zinafunikwa.

Nafasi

Nafasi ya sentimita 60 huachwa katikati ya mishororo na sentimita 20 katikati ya mimea.

Kupalilia

Kutoa kwekwe kunafaa kuanziwa wiki mbili baada kuchipuka na kwa maua ya kwanza na mara ya pili kufanywe punde tu kabla ya kuota maua.

Mbolea

Mbolea ya *Single* au *Triple super phosphate* inafaa kutiwa kwa kipimo cha kilo 20 hadi 25 kwa kila hekta.

Ulinzi wa mimea

Wadudu wanaoathiri:

Kabla ya kuota maua:

Aphids, thrips, leafhoppers

Baada ya kuota maua:

Aphids, wadudu wanaotoboa

mifuko ya mbegu, pod-

sucking bug na apion beetle

Bruchids na weevils

Wakati wa kuhifadhiwa:

Dawa aina kadha za kuzuia wadudu zinaweza kuzuia wadudu hawa. Dawa za kunyunyizia zinafaa kutiwa wakati ua linachipukizo, wakati maua yanawaviri na wakati mifuko ya mbegu inaundwa.

Kuvuna na uhifadhi

Mifuko yenye mbegu iliyokomaa inafaa kuvunwa ikiwa na rangi ya hudhuru na imeinama. Baada ya kutuo mbegu mifukoni, mbegu nilazima zikaushwe vyema kabla ya kuhifadhiwa.

Ili kuinga mbegu dhidi ya wadudu wanaoathiri mbegu zinapohifadhiwa, tia *super actellic dust* kiasi cha gramu 50 kwa kila gunia.

Majani ya muarubaini au majivu ya miti kiasi cha kilo 4 hadi 6 kwa kila gunia zinaweza kutumika pia.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Karanja, D. M'Ragwa, L. na Mutua, M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Katamani Research

S.L.P. 340, Machakos


Simu/Fax: 0202311449

Baruapepe: karikati@wananchi.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 12 / 2008

Shilingi Ishirini za Kenya

Ukuzaji kunde katika sehemu kame



Utangulizi

Kunde ni mmea ambao unatupatia majani mboga na pia mbegu ya chakula. Kunde hustahimili ukame na huchangia pakubwa katika kuzuia ukosefu wa chakula.


Aina za kunde na maumbile

Aina za kunde zinazopandwa sehemu kame na zile kavu kiasi ni M66, K80 na KVU27-1.

1. Machakos 66 (M66)

M66 ina majani mengi, hutambaa kiasi na hukuzwa kwa ajili ya mboga na mbegu.

- Majani na vijitawi ni vya kijani kibichi na maua ya zambarau na *corolla* nyeupe.
- Mifuko ya mbegu huwa kijani ikiwa changa, kisha inageuka kuwa myekundu mbegu ikijaa halafu ikawa hudhurungi-zambarau ikikauka.
- Huchukua muda wa siku 55 hadi 60 kutoa maua na kukomaa baada ya siku 80 hadi 90. Mazao yake hufikia kiwango cha kilo 800 hadi 1,700 kwa kila eka au kilo 312 hadi 680 kwa kila eka.
- Aina hii hustahimili virusi vya *yellow mottle na scab* na kwa kiwango kiasi hustahimili athari za *aphid* na *thrips*.



Machakos M66 (mazao za zambarau)

2. Katumani 80 (K80)

K80 hupandwa kwa matumizi ya mbegu na chakula.

- Hutambaa kiasi.
- Huwa majani marefu na vijitauri za kipekee vya rangi ya zambarau.
- Maua huwa na rangi ya zambarau, buluu na nyeupe pepepe.
- Mifuko ya mbegu ambayo haijakomaa ni ya rangi kijani, kasha hugeuka kuwa na wekundu kidogo uliochanganywa na hurudhurungi mifuko ikikomaa.
- Mazao yanaweza kufikia kiwango cha kilo 320 hadi mia 720 kwa kila eka
- Katumani hustahimili wadudu wa mimea (aphids) vyema, na kustahimili *thrips*, *pod borers* na *leafhopper*-kiasi.
- Katumani hustahimili maradhi ya majani ya kuvu kiasi.



Cowpea K80 (silvery mid rib)

3. KVU 27-1

Mbegu hii ina matumizi mawili, ya mbegu na majani na hutambaa wastani na maua yake yanachipuka na taratibu.

- Majani yake yana pembe kali.
- Maua yake yana rangi ya zambarau-buluu.
- Mbegu zina rangi yanyekundu.
- Mazao yake yanaweza kuwa kati ya kilo 320 na 720 kwa kila eka.
- Hustahimili wadudu wa *aphids na thrips*, wadudu watoboao mbegu, *leaf hoppers* na pia hustahimili maradhi ya *foliar fungal* na virusi vya *mosaic*.



KVU 27-1 (Majani yenye pembe kafi)

Utunzaji mimea

Utayarishaji ardhi

Unawoza kutimia mikono, jembe la kuvutwa na ng'ombe au tanga tanga.

Nyakati za kupanda

Zinahitaji kupandwa mapema baada ya kupata milimita 30 ya mvua.